

BUZZ FROM THE BEEHIVE

SILVERLEAF ACADEMY - USA RIVER CAMPUS

Wapendwa wazazi na walezi,

Tunafurahi kuwajua mambo mbalimbali na shughuli zilizo fanyika katika shule yetu kwa mwezi wa Februari. Kuanzia shughuli za kitaaluma na stadi za maisha ambazo huwajengea misingi mizuri wanafunzi wetu nje ya masomo ya kawaida. Jiunge nasi tunapoangazia kumbukumbu zilizounda mwezi uliopita na kutazama mambo mazuri yajayo.

MAMBO MUHIMU

Tunafurahi kuwajulisha kuwa, wanafunzi wetu walishiriki sherehe ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi, AICC Arusha. Wanafunzi wetu walionesha shauku yao na ujuzi wa juu kwa kuonesha jinsi mifumo ya umeme inavyofanya kazi, Tunayo furaha kuwajulisha kuwa Silverleaf Academy ni kati ya shule mbili pekee zilizoalikwa kushiriki katika maonesho haya. Tunatoa shukrani zetu za dhiti kwa chuo cha Nelson Mandela pamoja na Wizara na Elimu kwa mualiko huu ambao umeleta hamasa kubwa kwa wanafunzi wetu.



KUTOKA KWA WANAFUNZI

Kambi ya Skauti wilaya ya Arumeru ilifanyika tarehe 22 hadi 25 mwezi wa pili, katika kuadmimisha kumbukumbu ya kuzaliwa kwa muasisi wa Skauti duniani Sir Baden Powell, ambapo maadhimisho haya yalifanyika sehemu mbalimbali duniani. Lengo lingine la kambi hii ilikuwa ni Skauti kushirikiana katika kufanya shughuli mbalimbali za kijamii, kupata mafunzo ya uzalendo na kufanya usajili wa vijana wapya kujiunga na Skauti. Wanafunzi wetu walijifunza mambo mengi mazuri pamoja na kufahamiana na vijana wenzao kutoka shule mbalimbali.

**WANACHOJIFUNZA WANAFUNZI**

Lengo la kuwa na debate sio tuu kukuza lugha ya kiingereza, ila pia hujenga chachu ya uongozi, kujiamini na ushirikiano baina ya wanafunzi. Katika debate, wanafunzi hujifunza misamiati na maneno mapya, pamoja na kujenga ujuzi na ustadi wa lugha. Debate pia husaidia kujenga ushirikiano kati ya wanafunzi wanaposhiriki pamoja kujenga hoja. Kwa ujumla huwasaidia wanafunzi kupata ujuzi ambao utawasaidia katika taaluma na maeneo mengine katika maisha.



TIMU YETU INAJIFUNZA NINI?

Walimu wetu wamepata mafunzo maalum yaliyolenga kuboresha namna ya kufanya mabadiliko kati ya somo moja kwenda somo lingine, na pia usimamizi wa makundi ya wanafunzi (groups) katika ufundishaji kulingana na mazingira na mfumo wetu wa kujifunzia. Kwa kuzingatia umakini na namna bora ya kufanya mabadiliko hayo, walimu wetu sasa wamejengewa mikakati muhimu kuhakikisha mienendo (transition) isiyo na mkwamo, na kuwezesha wanafunzi wetu kuwa na siku nzuri katika masomo yao, kwa kuwa na utaratibu mzuri zaidi wa namna ya kuhama kutoka somo moja kwenda lingine, ama kati ya kikundi na kikundi.



DONDOO ZA KALENDA YA SHULE

Machi 20-21: Mitihani ya majaribio ya kati ya muhula: Machi 20-21

Machi 25: Kuanza kwa likizo ya katikati ya muhula.

Machi 29: Ijumaa Kuu

Machi 31: Sikukuu ya Pasaka

OMBI LETU KWENU

- Tufuate katika mitandao yetu ya kijamii ya Instagram na Facebook kwa ajili ya kupata taarifa na matukio za moja kwa moja pindi yanapotokea shuleni.



[@silverleafacademy_tz](https://www.instagram.com/silverleafacademy_tz)



[silverleafacademy](https://www.facebook.com/silverleafacademy)

- Tunawasihi kuendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa watoto wanapokua nyumbani. Timu yetu inahakikisha kuwa wewe na mtoto wako mnaendelea kupata huduma bora zaidi mwaka huu, hivyo kama utaona changamoto yoyote ama utakua na maswali na maoni ya namna tunaweza boresha huduma zetu, usisite kuwasiliana na mkuu wa shule ama ofisi yetu ya utawala wakati wowote.